
**Rais Henry B. Eyring**
Mshauri wa Kwanza katika
Urais wa Kwanza



# Amani katika Maisha Haya

Kwetu sote ambao tumezaliwa ulimenguni huu, Mwokozi alisema, "Ulimwenguni mnayo dhiki" (Yohana 16:33). Bado Yeye alitoa hii ahadi ya ajabu kwa wanafunzi Wake wakati wa huduma Yake duniani: "Amani nawaachieni; amani yangu nawapa; niwapavyo mimi sivyo kama ulimwengu utoavyo" (Yohana 14:27). Ni faraja kujua kwamba ahadi hii ya amani ya kibinafsi inaendelea kwa wafuasi Wake wote leo.

Baadhi yetu tunaishi katika mazingira mazuri na ya amani, na bado tunapatwa na vurugu za moyoni. Wengine wanahisi amani na utulivu kamili hata katika hasara kuu kibinafsi, janga, na majaribu yanayoendelea.

Unaweza kuwa uliona muujiza wa amani kwenye uso wa mfuasi wa Yesu Kristo ama kuisikia katika maneno yake. Nimeyaona haya mara nyingi. Wakati mwingine imekuwa katika chumba cha hospitali pale familia inapokusanyika kumzunguka mtumishi wa Bwana ambaye anakaribia kuaga.

Mimi nakumbuka kumtembelea mwanamke mmoja hospitalini siku chache kabla yeye kuaga kutokana na saratani. Mimi nilikuja pamoja na mabinti zangu wawili wadogo kwa sababu huyo dada mzuri wakati mmoja alipata kuwa mwalimu wao wa Msingi.

Wanafamilia wake walikuwa wamekusanyika kwenye kitanda chake, wakitamani kuwa pamoja naye katika dakika zake za mwisho duniani. Nilishangaa alipoinuka na kukaa kitandani. Aliwafikia mabinti zangu na kuwatambulisha wote, mmoja mmoja, kwa kila mwanafamilia wake. Alizungumza kana vile mabinti zangu walikuwa waheshimiwa wanaowasilishwa katika kitala cha malikia. Alikuwa na njia ya kusema kitu kumhusu kila mmoja chumbani, alikuwa mfuasi wa Mwokozi. Mimi bado ninakumbuka nguvu, uororo, na upendo katika sauti yake. Na nakumbuka kushangazwa na tabasamu yake yenye uchangamfu kwa vile alijua muda wake katika maisha haya ulikuwa mfupi.

Alikuwa amepokea baraka za ukuhani za faraja, na bado alitoa kwetu sote ushuhuda hai kwamba ahadi ya amani ya Bwana ni kweli: "Hayo nimewaambieni mpate kuwa na amani ndani yangu. Ulimwenguni mnayo dhiki; lakini jipeni moyo; mimi nimeushinda ulimwengu" (Yohana 16:33).

Alikuwa amekubali mwaliko Wake, kama vile sisi wote tunavyoweza, majaribu na shida zetu zozote.

"Njooni kwangu, ninyi nyote msumbukao na kulemewa na mizigo mizito, nami nitawapumzisha.

"Jifungeni nira yangu, na mkajifunze kwangu, maana mimi ni mpole na mnyenyekevu wa moyo, nanyi mtatulizwa rohoni mwenu" (Mathayo 11:28–29).

Ni tu kupitia Mwokozi ambapo kila mmoja wetu anaweza kupata amani na utulivu katika majaribu ambayo yatakuja kwetu sote.

Maombi ya sakramenti hutusaidia kujua jinsi ya kupata amani hiyo licha ya taabu za maisha. Tunapopokea sakramenti, tunaamua kuwa waaminifu kwa maagano yetu ya kumfuata Yeye.

Kila mmoja tunaahidi daima kumkumbuka Mwokozi.

Unaweza kuchagua kumkumbuka Yeye katika njia ambayo itauvuta moyo wako Kwake. Kwangu mimi wakati mwingine, ni kumuona Yeye katika akili yangu kama amepiga magoti katika Bustani ya Gethsemane ama kumuona Yeye akimwita Lazaro atoke nje kutoka kaburini. Ninapofanya hivyo, ninahisi ukaribu Naye na shukrani ambayo huleta amani kwenye moyo wangu.

Pia tunaahidi kutii amri Zake. Tunaahidi kuchukua jina Lake juu yetu na kuwa mashahidi Wake. Anaahidi kwamba unapoweka maagano yako Naye, Roho Mtakatifu atakuwa pamoja nawe. (Ona M&M 20:77, 79.)

Hii huleta amani katika angalau njia mbili. Roho Mtakatifu hututakasa kutoka kwa dhambi kwa njia ya Upatanisho wa Yesu Kristo. Na Roho Mtakatifu anaweza kutupatia amani ambayo huja kutokana na kuwa na idhinisho la Mungu na matumaini ya uzima wa milele.

Mtume Paulo asema kuhusu baraka hii ya ajabu: "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu" (Wagalatia 5:22).

Wakati malaika walipotangaza kuzaliwa kwa Mwokozi, walisema "Atukuzwe Mungu juu mbinguni, Na duniani iwe amani kwa watu aliowaridhia" (Luka 2:14; mkazo umeongezewa). Mimi natoa ushuhuda wangu kama shahidi wa Yesu Kristo kwamba Baba na Mwanawe Mpendwa wanaweza kumtuma Roho ili kutuwezesha kupata amani katika maisha haya, bila kujali majaribu yoyote ambayo yanaweza kuja kwetu na kwa wale tunaowapenda.

### KUFUNDISHA KUTOKA KWA UJUMBE HUU

Rais Eyring anafundisha kwamba maombi ya sakramenti yanaweza kutusaidia kujua jinsi ya kupata amani wakati wa majaribu yetu. Yanatukumbusha kwamba kama tutashika maagano yetu, tuna ahadi ya Mungu kwamba Roho Mtakatifu atakuwa pamoja nasi. Fikiria kuwauliza wale unaowafundisha jinsi kuwa na Roho Mtakatifu pamoja nasi kunatusidia kuwa na amani. Unaweza pia kushiriki mawazo yako ama uzoefu wa jinsi Roho Mtakatifu alivyowasaidia kuhisi amani wakati wa majabirbu. Unaweza kuwahimiza wale unaowafundisha watafakari juu ya ujumbe huu wakati wa sakramenti wiki hii.

© 2016 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa. Imepigwa chapa Marekani. Idhinisho la Kiingereza: 6/16. Idhinisho la Tafsiri: 6/16. Tafsiri ya *First Presidency Message, December 2016*. Swahili. 12872 743

## VIJANA

### Ni kwa Jinsi Utamkumbuka Mwokozi Wiki Hii?

Rais Eyring anatuhimiza "tuchague kumkumbuka [Mwokozi] katika njia ambayo itavuta moyo wako Kwake."

Je, "utamkumbuka Yeye vipi daima" wiki yote (ona M&M 20:77, 79)?

Je, una maandiko unayoyapenda yanayohusu Mwokozi? Unaweza kuweka alama maandiko tofauti kila siku wiki hii na kunyashiriki na mtu fulani.

Je, wewe huimba wimbo wa dini ama wimbo mwingine wa kuinua katika akili yako unapohisi kuzidiwa? Labda unaweza kuchagua mmoja mahususi unaohusu Mwokozi wiki hii.

Je, wewe utafakari kuhusu maisha ya Mwokozi na dhabihu yake ya upatanisho wakati wa sakramenti kila wiki? Unaweza kujiandaa kwa ajili ya sakramenti kwa kukumbuka chaguzi zako wiki yote ili daima kumkumbuka Mwokozi na kutubu kwa ajili ya wakati ulishindwa kufanya hivyo.

Je, unaomba kwa ajili ya nafasi za kushiriki injili kila siku? Jaribu kuwa na mazungumzo ya injili wiki hii ambayo yanazingatia Mwokozi. Unaweza kutoa ushuhuda juu ya Mwokozi wakati wa jioni ya familia nyumbani ama huongee na rafiki shuleni kuhusu uzoefu uliopata kanisa.

Weka lengo la kumkumbuka Mwokozi katika njia maalum wiki hii. Mwambie mzazi, ndugu, kiongozi, ama rafiki kuhusu lengo lako. Mwishoni mwa wiki, waambie kile kilichotokea. Utahisi vyote amani na furaha ambayo Rais Eyring alizungumza juu yake.

## WATOTO

### Njooni kwa Kristo

Mwokozi ametuahidi amani "tunapokwenda [Kwake]" (Mathayo 11:28). Hii inamaanisha kufuata mfano Wake na kujaribu kukaa karibu Naye.

- Kuwa na staha wakati wa skaramenti.
- Kuchagua kuwa mkarimu na kutowahukumu wengine.
- Kusoma kuhusu Mwokozi katika maandiko.

# Furaha ya Familia Inapatikana katika Wema

*Kwa maombi jifunze maneno haya na utafute msukumo wa kujua kitu cha kushiriki. Je, kuelewa "Familia: Tangazo kwa Ulimwengu" kutazidisha vipi imani yako katika Mungu na kubariki wale unaowachunga kupitia ualimu wa kutembelea? Kwa taarifa zaidi, nenda kwenye **www.reliefsociety.lds.org**.*

**Imani, Familia, Usaidizi**

Mungu "aliunda familia ili kutuletea furaha, kutusaidia kujifunza kanuni sahihi kwa njia ya upendo, na kutuandaa kwa ajili ya uzima wa milele."[1] Juu ya "mpango mkuu wa furaha" wa Mungu (Alma 42:8), Rais Russell M. Nelson, Rais wa Akidi ya Mitume Kumi na Wawili, alisema: "Mpango Wake unatangaza kwamba wanaume na wanawake wapo 'ili wapate shangwe' [2 Nefi 2:25]. Furaha hiyo huja wakati tunachagua kuishi katika uwiano na mpango wa milele wa Mungu."[2]

Nyumba ambayo Kristo ndiye kitovu huleta nafasi kuu za ufanisi. Mzee Richard G. Scott (1928–2015) wa Jamii ya Mitume Kumi na Wawili aliielezea kama mahali "ambapo injili inafundishwa, maagano yanashikwa, na upendo unazangaa," ambapo familia zinaweza kuishi "maisha ya utii" na kuwa "zimekita mizizi vyema katika injili ya Yesu Kristo."[3]

Rais Henry B. Eyring, Mshauri wa Kwanza katika Urais wa Kwanza, alisema: "Tunaweza kuamua kwamba tutafanya yale yote tunaweza ili kuzileta nguvu za mbinguni katika familia [yetu]." Na kuna uwezekano mwingi wa kudumisha upendo, huduma, utii, na furaha katika nyumba zetu kwa "[watoto wetu]" kulisikia neno la Mungu na kisha kulijaribu kwa imani." Ikiwa watafanya hivyo, asili yao itabadilika katika njia ambayo italeta furaha tunayotafuta."[4]

## *Nyumba Ambayo Kristo Ndiye Kitovu*

Tuna mifano mizuri ya Nyumba ambazo Kristo ndiye kitovu katika maandiko. Baada ya Lehi baba yake, kuaga, Nefi aliichukua familia yake na wengine ambao waliamini katika maonyo na manabii ya Mungu na wale ambao walisikia maneno ya Nefi kwenda mbali na nchi ya Walamani. Katika hii sehemu mpya, Wanefi wangeweza kutii hukumu, maagizo na amri za Bwana katika vitu vyote, kulingana na sheria ya Musa (ona 2 Nefi 5:6–10). Na bado miongoni mwa Wanefi, baadhi yao hatimaye wakawa si watiifu.

Na hali wanafamilia wetu wakati mwingine wanaweza kupotoka kutoka kwenye wema kama vile Wanefi walivyofanya, Mzee Scott alisema kwamba nyumba ambayo Kristo ndiye kitovu bado "inatoa uhakikisho mkuu wa amani na kimbilio katika nyumba zetu." Yeye alitambua kwamba "bado kuna changamoto au maumivu tele, lakini katikati ya vurugu, sisi tunaweza kufurahia amani ya moyo na furaha ya ajabu."[5]

## *Maandiko ya Ziada*

3 Yohana 1:4; 1 Nefi 8:12; 2 Nefi 5:27

**MUHTASARI**

1. *Handbook 2: Administering the Church* (2010), 1.1.4.
2. Russell M. Nelson, "Celestial Marriage," *Liahona,* Nov. 2008, 92.
3. Richard G. Scott, "For Peace at Home," *Liahona,* Mei 2013, 31.
4. Henry B. Eyring, "The Teachings of 'The Family: A Proclamation to the World,'" *New Era,* Sept. 2015, 5, 6.
5. Richard G. Scott, "For Peace at Home," 31.

### *Zingatia Hili*

Ni nini tunaweza kufanya ili kuishi kwa wema zaidi katika familia zetu?

© 2016 na Intellectual Reserve, Inc. Haki zote zimehifadhiwa. Imepigwa chapa Marekani. Idhinisho la Kiingereza: 6/16. Idhinisho la Tafsiri: 6/16. Tafsiri ya *Visiting Teaching Message, December 2016*. Swahili. 12872 743